# 7.0 KISWAHILI SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

**THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**

# KCPE 2014

1450422

## KISWAHILI
## SEHEMU YA KWANZA
## LUGHA

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI.**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ukiisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala **sio** katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba umeandika yafuatayo katika karatasi ya majibu:
   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**
5. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzoni mwa karatasi ya majibu.
6. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
7. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
8. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
9. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

   **Mfano:**
   **Katika kijitabu cha maswali:**

   **21.** Chagua jibu lenye ala za muziki pekee.
   A. filimbi, udi, mvukuto, chapuo
   B. njuga, tari, kinubi, fidla
   C. harimuni, marimba, msondo, maleba
   D. siwa, zeze, upatu, nembo.

   Jibu sahihi ni B

   **Katika karatasi ya majibu:**

   1 [A] [B] [C] [D] 11 [A] [B] [C] [D] 21 [A] ~~[B]~~ [C] [D] 31 [A] [B] [C] [D] 41 [A] [B] [C] [D]

   Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **21**, kisanduku chenye herufi **B** ndicho kilichochorwa kistari.
10. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
11. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

904504

© *The Kenya National Examinations Council, 2014*

**GEUZA UKURASA**

**Maswali 1 mpaka 15.**

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi **1** mpaka **15**. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.*

Usalama ni jambo **1** kudumishwa kwa dhati; yaani **2**. Wizara husika **3** kiasi maalum cha fedha kwenye bajeti ya taifa ili kugharamia shughuli za usalama. **4** shughuli hizi ni kuwapa askari **5** za kukabiliana na wakiuka sheria. **6**; uhifadhi wa usalama haupaswi kuachiwa polisi na wanajeshi pekee. Kila mwananchi sharti awajibike kupalilia amani; si kwa heri, si kwa shari, si kwa fanaka, si kwa **7**; wanajamii wote **8** kukabiliana kila wakati na mtu yeyote anayezua vurugu.

**1.** A. linaostahili B. unaostahili C. linalostahili D. unalostahili

**2.** A. kwa uaminifu B. kwa nia C. kwa ustadi D. kwa hamu

**3.** A. ikitengewa B. ingetengewa C. inatengewa D. ikatengewa

**4.** A. Baadhi ya B. Kati ya C. Mkabala na D. Pamoja na

**5.** A. hekima B. mikakati C. ilhamu D. stadi

**6.** A. Papo kwa papo kamba hukata jiwe B. Chombo hakiendi ila kwa kafi C. Bahari haivukwi kwa kuogelea D. Kinga na kinga ndipo moto uwakapo

**7.** A. ukosefu B. shauku C. sikitiko D. uchungu

**8.** A. wapige darubini B. wakae ange C. wakae tutwe D. wapige hema

Mweledi alipojiunga na shule ya chekechea walimu wake walitambua kuwa alikuwa na kipawa cha **9**. Baada ya muhula mmoja tu, aliweza kusimama jukwaani kukariri na kughani mashairi ya **10**, yaani yenye mishororo mitatu katika kila ubeti; walimu na wanafunzi wenzake wakawa ndio **11** yake. Walimu walimpa mazoezi zaidi ili **12**. Kadhalika, Mweledi **13** masomo kiasi kwamba katika darasa la tano aliweza kutambua aina za vivumishi kama vile: **14**, pamoja na akisami kama sudusi tatu ambayo kwa tarakimu ni **15**.

**9.** A. kigeni B. kipekee C. kihalali D. kiasili

**10.** A. tathnia B. tarbia C. tathlitha D. takhmisa

**11.** A. halaiki B. msoa C. mashabiki D. hadhira

**12.** A. aimarike B. waimarishe C. aimarishe D. waimarike

**13.** A. aliuthamini B. alizithamini C. aliyathamini D. aliithamini

**14.** A. ajabu, mwema, jepesi B. hodari, tano, matamu C. kiasi, tena, vile D. lake, laini, mno

**15.** A. $\frac{6}{3}$ B. $\frac{9}{3}$ C. $\frac{3}{6}$ D. $\frac{3}{9}$

*Kutoka swali la **16** mpaka **30**, chagua jibu lililo sahihi.*

**16.** Kukanusha kwa: 'Mtumbwi ambao ulinunuliwa umeanza safari', ni:
A. Mtumbwi ambao ulinunuliwa haukuanza safari.
B. Mtumbwi ambao haukununuliwa haujaanza safari.
C. Mtumbwi ambao ulinunuliwa haujaanza safari.
D. Mtumbwi ambao haukununuliwa haukuanza safari.

**17.** Chagua usemi halisi wa sentensi ifuatayo: Mwenesi alimwambia ndugu yake kuwa wangeenda Mombasa siku ambayo ingefuata.
A. "Kesho mtaenda Mombasa." Mwenesi alimwambia ndugu yake.
B. "Siku iliyofuata mlienda Mombasa." Mwenesi alimwambia ndugu yake.
C. "Kesho utaenda Mombasa." Mwenesi alimwambia ndugu yake.
D. "Siku iliyofuata ulienda Mombasa." Mwenesi alimwambia ndugu yake.

**18.** Chagua wingi wa sentensi ifuatayo: Mruka kiunzi alipongezwa aliponyakua nishani hiyo.
A. Waruka viunzi walipongezwa waliponyakua nishani hiyo.
B. Waruka viunzi walipongezwa waliponyakua nishani hizo.
C. Mruka viunzi alipongezwa aliponyakua nishani hiyo.
D. Mruka viunzi alipongezwa aliponyakua nishani hizo.

**19.** Ikiwa mtondogoo itakuwa Jumanne, leo ni:
A. Jumamosi
B. Alhamisi
C. Ijumaa
D. Jumatano.

**20.** Chagua sentensi yenye kiwakilishi kimilikishi.
A. Mzazi wake alihudhuria sherehe lakini wangu hakuhudhuria.
B. Mtoto wao aliamka mapema lakini huyu alichelewa.
C. Mfanyakazi wa tatu alistaafu lakini wengine walibakia.
D. Msafiri wa nne alipata kibali lakini wale hawakupata.

**21.** Natu ameolewa na John. Dada yake Natu ameolewa na Ken. Ken na John wataitana:
A. mwamu
B. mwanyumba
C. kivyere
D. mkwe.

**22.** Ni kundi lipi lenye viunganishi pekee?
A. maadamu, kama, kefule, hamadi
B. ijapokuwa, ila, wala, bali
C. labda, ingawa, ikiwa, hata
D. sembuse, tangu, badala, basi.

**23.** Shehena ni ya mizigo ilhali _____________ ni la udongo.
A. tita
B. peto
C. shumbi
D. bumba.

**24.** Chagua sentensi yenye maelezo sahihi.
A. Hijabu ni ugonjwa wa kuvimba fizi.
B. Kimeta ni ugonjwa unaodhoofisha figo.
C. Tauni ni ugonjwa unaokatakata viungo.
D. Surua ni ugonjwa wa kutoa vipele.

**25.** Ni sentensi ipi yenye matumizi sahihi ya koloni?
A. Jumapili ni tarehe: 3.3.2012.
B. Mama alinunua matunda: yaani, chungwa, fenesi na embe.
C. Teknolojia imefanikisha maendeleo: akasema waziri.
D. Miji niliyotembelea ni hii: Kisumu, Nairobi, Voi na Embu.

**26.** Gugu ni nyasi ndefu zinazomea katika sehemu tambarare, gugu pia ni _____________
A. mmea unaotambaa kote shambani;
B. mmea unaobana mingine shambani;
C. mmea unaomea pale pasipopaliliwa;
D. mmea unaomea mahali usipotakikana.

**27.** Chagua jibu lenye maelezo sahihi.
A. Mjumu ni fundi wa kufua visu.
B. Sogora ni bingwa wa kuimba mashairi ngomani.
C. Dalali hushindania bidhaa mnadani.
D. Mkalimani hutafsiri maandishi vitabuni.

**28.** Sentensi, 'Jedi ni ninga' imetumia tamathali gani?
A. Msemo
B. Tashbihi
C. Sitiari
D. Nahau.

**29.** Arbuni ni _____________
A. sehemu ya bei ya kitu inayotolewa mwanzoni;
B. sehemu ya ujira wa kumsaidia mtu mwanzoni;
C. sehemu ya fidia anayolipwa mtu mwanzoni;
D. sehemu ya malipo ya kukopea kitu mwanzoni.

**30.** Methali, 'Kamba ya mbali haifungi kuni', ni kwa wanaotegemea msaada wa walio mbali. 'Maji ya kifuu bahari ya chungu', ni kwa:
A. anayeiona hadhi ya vitu kuwa ya chini;
B. anayeyaona matatizo ya wengine kuwa madogo;
C. anayeziona hali za wengine kuwa za kawaida;
D. anayeviona vitu vidogo kuwa na faida chache.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **31** mpaka **40**.*

Afya au siha ni hali ya kutokuwa na maradhi. Hali hii humwezesha mtu kuhifadhi nguvu zake za mwili na kufanikisha utendakazi katika nyanja tofautitofauti. Mtu mwenye afya bora huweza kutekeleza mengi bila udhia. Mathalani, yeye huweza kujirausha na kujishughulisha hadi jioni bila kuhisi uchovu mwingi.

**Mti hauendi ila kwa nyenzo**, nayo afya nzuri haimjii tu mtu. Afya hustahili kupaliliwa na kutunzwa kwa namna anuwai kama vile kula vyakula vyenye viinilishe, kufanya mazoezi na kuandama mienendo miadilifu. Usafi wa mwili na mazingira pia huchangia katika kuimarisha afya. Ni wazi kwamba mazingira yakiwa machafu hukosa kuvutia na kusababisha kuhanikiza kwa harufu **inayokirihisha**. Isitoshe, uchafu huwa hali mufti ya kuzaana kwa wadudu kama vile chawa, kunguni, nzi na mbu ambao ni maadui wakuu wa afya.

Tabia ya mja huathiri afya yake. Wapo watu ambao wameambulia magonjwa kama vile saratani ya ini na mapafu, na kifua kikuu kutokana na uraibu wa pombe, sigara na dawa za kulevya. Wengine hujiponza kwa kuingilia vitendo viovu kama vile kushiriki mapenzi kiholela na kujisababishia magonjwa. Magonjwa haya ni kama vile kaswende na ukimwi ambao umewapukutisha wengi.

Hali kadhalika, watu hujiharibia afya kwa kufanya kazi mfululizo bila kupumzika. Licha ya kwamba bidii ni muhimu katika maendeleo ya jamii yoyote ile, utendaji kazi kidindia huweza kuwa na athari hasi. Kuna baadhi ya watu ambao wamewahi kupata maradhi ya moyo, ya kiakili na hata shinikizo la damu kutokana na hali kama hii. Wengine hujihasiri kwa kula vyakula vingi kupindukia. Kadhalika, wapo wengine ambao hupata magonjwa kwa kula vyakula visivyofaa. Katika kundi hili kuna wale ambao hawadiriki kufanya kazi wala mazoezi. Hawa hujinenepea na kudhoofisha utendakazi wao. Pia kuna wengine ambao hawali chakula cha kutosha. Hawa nao huweza kupata magonjwa kama vile safura na vidonda vya tumbo.

Hali ya umaskini pia huchochea kuzoroteka kwa afya. Asilimia kubwa ya watu nchini humu haimudu huduma bora za afya na lishe bora kutokana na hali ya ufukara. Wengine, kwa kukosa fedha, hawapati elimu ya kimsingi kuhusu afya. Hawa huweza kujizulia magonjwa kwa kutojua na kutofuata kanuni za afya. Pamoja na haya, kuna wale ambao wanarithi magonjwa ya kiukoo kama vile bolisukari kutoka kwa wazee wao.

**Umuhimu wa afya hauwezi kupuuzwa.** Taifa lenye kizazi chenye afya hustawi kiuchumi. Afya ikidumishwa wanajamii huweza kutumia fedha zao kuwekeza katika miradi badala ya kuzitumia kujiuguza au kuwauguza wenzao. Ni jukumu la kila raia kuhakikisha kwamba ameilinda afya yake na ya wengine kwa vyovyote vile. Walio na mazoea ya kupuuza ushauri wa wanaotoa huduma za afya na lishe wajiase, la sivyo watakuja kujiuma vidole.

**31.** Kulingana na aya ya **kwanza**, afya:
A. huimarisha matokeo ya utendakazi;
B. humwondolea mtu matatizo mwilini;
C. humpunguzia mtu mazoea ya uchovu;
D. hukuza maendeleo katika maeneo mbalimbali.

**32.** Ni muhimu kutunza mazingira kwani:
A. tutarudisha hali ya kupendeza;
B. tutaepuka kuenea kwa harufu;
C. tutamaliza vikwazo tofautitofauti vya afya;
D. tutazuia ongezeko la wadudu waharibifu.

**33.** Mwandishi anapinga hali gani **hasa** katika aya ya **tatu**?
A. vifo vya watu wengi;
B. kuhusiana bila mpango;
C. matumizi mabaya ya vileo;
D. uambukizaji wa magonjwa.

**34.** Chagua jibu ambalo **si sahihi** kulingana na aya ya **nne**.
A. Jambo jema huweza kusababisha madhara.
B. Kazi nyingi husababisha ugonjwa wa moyo.
C. Mazoezi hudhibiti ukubwa wa mwili.
D. Mapumziko huimarisha hali ya mtu kiakili.

**35.** Chakula huwadhuru:
A. wanaokula mara zote na kunenepa jinsi isivyostahili;
B. wasiofanya juhudi kuongeza hamu ya kazi;
C. wasiopanga njia nyingi za kutumia lishe;
D. wanaokula kiasi kisicholingana na mahitaji yao kimwili.

**36.** Chagua jibu sahihi kulingana na kifungu.
A. Watu wengi nchini hupata magonjwa kutoka kwa jamaa zao.
B. Watu wengi nchini hudhoofika kiafya kwa kukosa pesa.
C. Watu wengi nchini hawajui hali ya afya zao.
D. Watu wengi nchini hupuuza onyo kuhusu afya.

**37.** **Umuhimu wa afya hauwezi kupuuzwa** kwa vile:
A. Magonjwa husababisha kuzorota kwa maendeleo.
B. Watu wagonjwa hawawezi kuizalisha mali.
C. Pesa nyingi hutumiwa kuwatunza walio hospitalini.
D. Mipango nchini hukwama wahudumu wakikosekana.

**38.** Chagua funzo linalojitokeza katika aya ya mwisho.
A. Taifa haliwezi kuimarisha afya bila raia wote kuhusika.
B. Wanaodharau watu wenye busara hupata maradhi.
C. Mtu hawezi kufaidika kiafya bila kupata ushauri.
D. Wanaokosa kujikanya hupata majuto baadaye.

**39.** Maana ya, **'mti hauendi ila kwa nyenzo'** imejitokeza vipi katika kifungu?
A. Wanaokula vyakula vyenye viinilishe huzuia kunenepa.
B. Wanaoepuka kazi hawapati shinikizo la damu.
C. Wanaozingatia mienendo mizuri hudumisha afya.
D. Wanaonyoosha viungo vyao huwa wakakamavu.

**40.** Maana ya **'inayokirihisha'** ni:
A. inayodhuru;
B. inayoenea;
C. inayoaibisha;
D. inayochukiza.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **41** mpaka **50**.*

Shawe alizaliwa katika familia iliyojiweza. Malezi yake basi yangeweza kutabiriwa. **Alilelewa kwa tunu na tamasha, asijue maana ya msamiati wa kukosa.** Wazazi wake walikuwa wafanyabiashara maarufu ambao walisafiri nchini na ng'ambo kwa shughuli hizo. Hata hivyo, hawakukosa muda wa kutangamana na mwanao. Walimwelekeza na kumfunza maadili na kanuni za kijamii, si kwa maneno tu, bali pia kwa vitendo.

Miongoni mwa mambo ambayo wazazi wa Shawe walitilia maanani ni umoja na mshikamano wa kijamii. Pamoja na kwamba walikuwa kiguu na njia katika kujiinua kiuchumi, hakuna sherehe ya kijijini, iwe harusi au matanga waliyokosa kuhudhuria. Wakati ambao mmoja wao alikuwa safarini, mwenzake alimwakilisha. Wanakijiji waliwapenda na kuwastahi, nao wakawa hawaishi kumsifia Shawe ukarimu na uchangamfu wa wanakijiji. Walimshauri kuhusu umuhimu wa kushirikiana na wengine na kumtahadharisha kuwa mtu pweke ni uvundo.

Shawe aliendelea kukua, akarithi tabia ya wazazi wake ya kuinamia cha mvunguni; akawa mwanafunzi bora masomoni, tena mtiifu kwa walimu na hata majirani. Bidii yake ilizaa matunda, akapanda ngazi moja hadi nyingine kielimu, akafikia kilele cha elimu yake chuoni alipohitimu shahada ya tatu. Baadaye alipata kazi nzuri na kupanda madaraka kutokana na bidii yake. Baada ya kudunduliza pesa za kutosha za kuikimu familia, Shawe aliamua kuoa. Hapa ndipo maisha yake yalipochukua mkondo mwingine.

Shawe alijikuta amekabiliwa na mabadiliko ya kihali ambayo hakuyawazia. Awali alikuwa akiwategemea wazazi kwa ushauri na maelekezo, sasa ndiye aliyetarajiwa kuwa mshauri na mwelekezi wa familia yake. Majukumu mengine ya kijamii pia yalimtumbulia macho. Pamoja na shughuli nyingi za kikazi, desturi za jamii yake zilimhitaji kushirikiana na wanajamii wenzake kwa hali na mali. Ingawa Shawe alikuwa mkono wazi, alihisi kuwa hakuwa na muda wa kutosha kutangamana na wanajamii wenzake katika shughuli kama vile kudumisha usalama, sherehe za posa na hafla za kuchangia elimu ya watoto maskini.

Mkewe Shawe alijaribu kumrai atenge muda, hasa mwishoni mwa wiki, kuingiliana na wanajamii wengine lakini kila mara Shawe alilalamikia hili na lile akisema kwamba ametingwa na kazi. Palipotokea haja ya kifedha, Shawe hakuchelewa kutoa mchango wake. Hakika hata alitoa pesa kila mwezi kukuza hazina ya Chama Cha Masilahi Ya Mtaa alikoishi. Mkewe alikerwa mno na hali hii na kumkumbusha kila mara kuwa pesa hununua; hazitumwi. Wanakijiji nao, pamoja na kwamba walitambua na kuienzi michango yake ya kifedha, walihisi kwamba Shawe anajitenga nao. Kulingana nao, Shawe aliwanyima fursa ya kufaidika kwa kipawa chake cha uongozi. Walimtumia mjumbe, si mara moja, si mara mbili kuhusu hali hii. Shawe ambaye alikuwa amedidimia zaidi katika kazi yake alikiona kitendo cha wanakijiji kama usumbufu. **"Mimi hutuma michango yangu kila mara wanapoihitaji, wanataka nini zaidi?"** alisema Shawe.

Siku moja Shawe alikuja kutambua maana ya methali, 'Kinyozi hajinyoi'. Kifungua mimba wake aliamua kuuasi ukapera, akamtaka babake kupeleka posa kwa mchumba wake. Kama ilivyokuwa desturi, Shawe alihitaji kuandamana na wazee na akina mama katika shughuli hii. Alimtuma mkewe kumjuza kinara wa baraza la ukoo pamoja na mwenyekiti wa Chama Cha Masilahi Ya Mtaani. Viongozi hawa walipopata ujumbe huo, walitabasamu tu, wakawakusanya wanachama wao kuwapasha habari, wanachama wakafurahi kwamba mtoto anapata jiko. Walikusanya pesa na kumtumia Shawe kupitia kwa mkewe huku kila mmoja wao akituma udhuru wa kutohudhuria. Shawe alipokea bahasha iliyosetiri kibunda cha pesa kutoka kwa mkewe, akazitazama kwa masikitiko makuu huku amejiinamia kwa fedheha. Lilikuwa pigo lililohitaji moyo wa jiwe kulikabili.

**41.** Wazazi wa Shawe walikuwa walezi wema kwa vile:
A. walikuwa kielelezo chema kwa Shawe;
B. waliweza kuzingatia desturi za kijamii;
C. walifanya bidii katika biashara yao;
D. walisema na Shawe bila shida.

**42.** Kifungu kinaonyesha kwamba:
A. Shawe alibainisha umuhimu na uwezo wa wanakijiji.
B. Wazazi wa Shawe waliungana na wanakijiji katika hali zote.
C. Wazazi wa Shawe walifurahia kutangamana kwa wanakijiji.
D. Shawe alijifunza maana ya ushirikiano kwa namna zote.

**43.** Shawe alifanana vipi na wazazi wake?
A. Aliwaheshimu walimu na majirani.
B. Alipiga hatua moja hadi nyingine maishani.
C. Aliweka akiba hadi akaoa kwao kijijini.
D. Alijitahidi masomoni na kazini.

**44.** Kulingana na aya ya **nne**, jamii:
A. Inamhitaji kila mmoja kukumbuka maendeleo ya kijamii.
B. Inamhitaji kila mmoja kushiriki kuendeleza elimu ya kijamii.
C. Inamhitaji kila mmoja kuhusika katika kanuni za kijamii.
D. Inamhitaji kila mmoja kuzipenda shughuli za kijamii.

**45.** Chagua maoni ya wanakijiji kumhusu Shawe.
A. anayeweza kuboresha uendeshaji wa kijiji;
B. aliyejaliwa mali pamoja na utu;
C. aliyependa kutoa usaidizi wake haraka;
D. anayejua kuangazia masuala ya jamii.

**46.** **"Mimi hutuma michango yangu kila mara wanapoihitaji, wanataka nini zaidi?"**, inaonyesha kuwa:
A. Wanakijiji walimtarajia Shawe kuwafikiria ipasavyo.
B. Wanakijiji waliutarajia ushirika kamili wa Shawe.
C. Wanakijiji walimtarajia Shawe kuwaandama vilivyo.
D. Wanakijiji waliutarajia uelekezi ufaao wa Shawe.

**47.** Wanakijiji wanajaliana masilahi **hasa** kwa kuwa:
A. Walimwonya Shawe kuhusu upuuzaji wa ushirikiano.
B. Walimpa mkewe Shawe pesa ashughulikie ndoa.
C. Walizingatia ubora wa hazina ya chama.
D. Walichangamkia vyema ndoa ya mwanawe Shawe.

**48.** Wazo **kuu** linalojitokeza katika aya ya mwisho ni kwamba;
A. Wanakijiji walikuwa wamenuia kumpuuza Shawe.
B. Wanakijiji walikuwa wameudhika na ujumbe wa Shawe.
C. Wanakijiji walikuwa wamechoshwa na kupotoshwa kwa Shawe.
D. Wanakijiji walikuwa wameamua kumrekebisha Shawe.

**49.** Kwa nini **hasa** Shawe alijitenga na wanakijiji?
A. kukerwa;
B. kutosheka;
C. kiburi;
D. kisomo.

**50.** Chagua maana ya kifungu kifuatacho:
**'Alilelewa kwa tunu na tamasha, asijue maana ya msamiati wa kukosa.'**
A. alipendwa na kutimiziwa mahitaji yake yote;
B. alipendwa na kurithishwa yote aliyoyataka;
C. alipendwa na kuonyeshwa yaliyomfaa kwao;
D. alipendwa na kushauriwa kuhusu hali yake.

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# KCPE 2014

1450523

## KISWAHILI
## SEHEMU YA PILI
## INSHA

**Muda: Dakika 40**

| | |
|---|---|
| **NAMBA YAKO YA MTIHANI** | |
| **JINA LAKO** | |
| **JINA LA SHULE YAKO** | |

**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI.**

1. Kwenye nafasi zilizoachwa hapo juu, andika Namba yako kamili ya mtihani, Jina lako na Jina la Shule yako.

2. Sasa geuza ukurasa huu. Soma kichwa cha insha kwa makini kisha uandike insha yako kwenye nafasi ulizoachiwa.

3. Insha **lazima** iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

**Kijitabu hiki kina kurasa 4 zilizopigwa chapa.**

904505

*© The Kenya National Examinations Council, 2014*

**GEUZA UKURASA**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.

Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:

Huyo alikuwa ndugu ambaye kamwe sitaweza kumsahau.